



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA
NYANG'HWALE**

25.10.2022

**TANGAZO LA USAFI WA MAZINGIRA WA KILA JUMAMOSI YA MWISHO
WA MWEZI**

MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA YA NYANG'HWALE ANAWATANGAZIA WANANCHI NA WAKAZI WOTE WA WILAYA YA NYANG'HWALE KUFANYA USAFI WA MAZINGIRA SEHEMU ZA MAKAZI NA BIASHARA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI OKTOBA TAREHE 29/10/2022 KUANZIA SAA 1.30 ASUBUHI HADI SAA 3.30 ASUBUHI.

- TAKA ZOTE ZIKUSANYWE NA KUCHOMWA MOTO AU KUFUKIWA.
- NYASI KATIKA MAENEO YA MAKAZI ZIFYEKWE AU KUSESWA.
- VIWANJA NA MAPAGALA AMBAYO HAYAJAENDELEZWA YASAFISHWE.
- VYOO BORA VIJENGWE NA VITUMIKE VIZURI.
- VYANZO VYA MAJI VISAFISHWE, VITUNZWE NA VILINDWE.
- USAFI WA MAZINGIRA KIWILAYA UTAFANYIKA KATIKA KATA YA KABOHA (SHIBALANGA).

**SHUGHULI ZOTE ZA BIASHARA ZIFUNGWE HADI SAA 3.30 ILI KUTOA
MWANYA WA WATU KUFANYA USAFI WA MAZINGIRA.**

FAINI YA PAPO HAPO YA **SH. 50,000/=** KWA YEYOTE AMBAYE HATAZINGATIA AGIZO HILI NA ATAKAYEKUTWA AKIISHI KATIKA MAZINGIRA MACHAFU.

"MAZINGIRA SAFI NI AFYA BORA"

ps
MWIZARUBI NYAINDI
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NYANG'HWALE.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S. L. P. 352, Mkoa wa Geita, Barua
pepe:ded@nyanghwaledc.go.tz Tovuti: www.nyanghwaledc.go.tz